JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA MASWALI YA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA) 2021

MAARIFA YA JAMII

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA MASWALI YA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA) 2021

03 MAARIFA YA JAMII

Kimechapishwa na;

Baraza la Mitihani la Tanzania,

S.L.P. 2624,

Dar es Salaam, Tanzania.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2021

Haki zote zimehifadhiwa

YALIYOMO

DIBAJI iv

1.0 UTANGULIZI 1

2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA KILA SWALI . 2

2.1 Sehemu A: Maswali ya Kuchagua na Kuoanisha 3

2.1.1 Swali la 1: Kutambua matukio yanayotokea katika mazingira yanayomzunguka. 3

2.1.2 Swali la 2: Kufuata Kanuni za Kiuchumi katika Shughuli za Uzalishaji Mali 13

2.2 Sehemu B: Maswali ya Majibu Mafupi 20

2.2.1 Swali la 3: Kutambua Misingi ya Uzalendo katika Jamii. 20

2.2.2 Swali la 4: Kutumia Ramani na Elimu ya Anga katika Maisha ya kila Siku 31

3.0 TATHIMINI YA KUFAULU KWA KILA UMAHIRI 37

4.0 HITIMISHO 38

5.0 MAPENDEKEZO 39

KIAMBATISHO 40

DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa Taarifa ya Uchambuzi wa Majibu ya Maswali ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne (SFNA, 2021) kwa somo la Maarifa ya Jamii. Lengo la taarifa hii ni kutoa mrejesho kwa wanafunzi, walimu, watunga sera, wakuza mitaala na wadau wengine wa elimu kuhusu stadi na kwa kiwango gani wanafunzi waliweza kujifunza, au kutojifunza katika kipindi cha miaka minne ya Elimu ya Msingi.

Katika taarifa hii, mambo ambayo yamechangia ufaulu wa wanafunzi katika kila swali yameainishwa. Uchambuzi unaonesha kuwa ufaulu mzuri wa wanafunzi katika maswali umetokana na uelewa mzuri wa mahitaji ya kila swali, na kuwa na umahiri wa kutosha katika somo. Pamoja na hayo, wanafunzi ambao hawakufaulu vizuri ni wale ambao wameshindwa kutambua mahitaji ya maswali kutokana na umahiri mdogo katika stadi za kusoma na kuandika. Wanafunzi wengine hawakuwa na umahiri katika maeneo yaliyotahiniwa.

Uchambuzi wa ufaulu wa wanafunzi katika kila umahiri ulifanyika na kuonesha kuwa, wanafunzi wamefanya vizuri katika umahiri wa *Kutambua Matukio Yanayotokea katika Mazingira Yanayomzunguka, Kufuata Kanuni za Kiuchumi katika Shughuli za Uzalishaji Mali na Kutumia Ramani na Elimu ya Anga katika Maisha ya Kila Siku.* Kwa upande mwingine, umahiri wa *Kutambua Misingi ya Uzalendo katika Jamii* ulikuwa na ufaulu hafifu.

Baraza la Mitihani la Tanzania linatarajia kuwa, mrejesho unaotokana na ripoti hii utaziwezesha mamlaka mbalimbali za elimu kuchukua hatua madhubuti ili kuboresha michakato ya ufundishaji na ujifunzaji. Pia, Baraza linatarajia kuwa changamoto zilizochangia ufaulu usioridhisha katika baadhi ya umahiri zinatatuliwa ili kuongeza ufaulu kwa wanafunzi wanaotarajiwa kuingia darasa la tano.

Baraza la Mitihani la Tanzania linapenda kutoa shukrani za dhati kwa wote waliohusika katika kuandaa taarifa hii.

Dr. Charles E. Msonde
KATIBU MTENDAJI

1.0 UTANGULIZI

Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne (SFNA, 2021) ulifanyika tarehe 28 na 29 Oktoba 2021. Jumla ya watahiniwa 1,681,769 (100%) walisajiliwa kufanya upimaji katika somo la Maarifa ya Jamii. Watahiniwa 1,560,856 (92.81%) walifanya upimaji ambapo watahiniwa 1,425,478, sawa na asilimia 91.33% walifaulu.

Karatasi ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne katika somo la Maarifa ya Jamii ilikuwa na maswali manne (04). Maswali haya yaligawanywa katika sehemu kuu mbili; A na B. Sehemu A ilikuwa na maswali 2 ambayo ni; swali la 1 na 2 yenye jumla ya vipengele 14 kutoka katika mahiri kuu mbili. Swali la 1 lilipima umahiri wa *Kutambua Matukio Yanayotokea katika Mazingira Yanayomzunguka* na umahiri wa *Kufuata Kanuni za Kiuchumi katika Shughuli za Uzalishajimali* kilipimwa katika swali la 2. Sehemu B ilikuwa na maswali mawili, swali la 3 na 4 yenye jumla ya vipengele 11. Maswali haya yalitoka katika mahiri kuu mbili ambazo ni; *Kutambua Misingi ya Uzalendo katika Jamii* na *Kutumia Ramani na Elimu ya Anga katika Maisha ya kila Siku*. Wanafunzi walitakiwa kujibu maswali yote kutoka sehemu zote mbili. Kwenye sehemu A swali la 1, wanafunzi walitakiwa kuchagua herufi ya jibu sahihi na kuiandika katika kisanduku. Katika swali la 2, wanafunzi walitakiwa kuoanisha changamoto za shughuli za kiuchumi zilizopo katika fungu A na aina ya shughuli za kiuchumi katika fungu B, kisha kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano. Katika sehemu B swali la 3, wanafunzi walitakiwa kusoma kifungu cha habari na kisha kujibu maswali yaliyofuata, wakati swali la 4 wanafunzi walitakiwa kusoma ramani na kisha kujibu maswali yaliyofuata.

Katika taarifa hii, utangulizi unafuatiwa na uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika kila swali. Uchambuzi unabainisha umahiri wa wanafunzi, ukiambatana na majibu yao ambayo ama yalikuwa ya kiwango kizuri, cha wastani, au hafifu kulingana na swali husika. Sababu za kila kundi kuwa na umahiri waliouonesha pia zimechambuliwa. Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika kila swali umefuatiwa na tathimini ya ufaulu wa wanafunzi katika kila umahiri. Sehemu hiyo imefuatiwa na hitimisho na baadaye mapendekezo yatakayotokana na uchambuzi uliofanyika.

Viwango vya ufaulu wa wanafunzi vimezingatia asilimia ya wanafunzi waliofanya swali husika. Iwapo watahiniwa kati ya asilimia 0 hadi 33 tu ndio walioweza kujibu swali hilo vizuri, kiwango hiki cha ufaulu kilihesabika kuwa ni **hafifu***.* Kwa upande mwingine, kama wanafunzi walioweza kujibu swali hilo vizuri ni kati ya asilimia 34 hadi 66, ufaulu huo ulihesabika kuwa ni wa ***wastani.*** Pia, kiwango cha kufaulu kilihesabika kuwa ni ***kizuri*** iwapo wanafunzi walioweza kufanya swali hilo vizuri ni kati ya asilimia 67 hadi 100. Katika uchambuzi huu, rangi ya kijani, njano na nyekundu zimetumika kuonesha ufaulu mzuri, wastani na hafifu mtawalia.

2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA KILA SWALI

Kwa ujumla, uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa, kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi kilikuwa kuzuri katika swali la 1 na la 2, cha wastani katika swali la 4, na hafifu katika swali la 3. Katika sehemu hii, kila swali limechambuliwa na utendaji wa wanafunzi kubainishwa. Vielelezo vimetumika kuthibitisha hoja zilizotolewa katika kila swali.

2.1 Sehemu A: Maswali ya Kuchagua na Kuoanisha

Sehemu hii iliundwa na maswali mawili yenye jumla ya vipengele 14. Swali la 1 lilikuwa na vipengele nane vya maswali ya kuchagua. Mwanafunzi alitakiwa kusoma swali, na kisha kuchagua jibu sahihi kutoka katika machaguo aliyopewa. Swali la pili lilikuwa la kuoanisha ambalo lilikuwa na vipengele sita. Mwanafunzi alitakiwa kusoma maswali kutoka fungu A, na kuoanisha na jibu sahihi kutoka fungu B.

2.1.1 Swali la 1: Kutambua Matukio Yanayotokea katika Mazingira Yanayomzunguka

Swali hili lilikuwa na vipengele nane (i) hadi (viii) vilivyopima umahiri wa *Kutambua Matukio Yanayotokea katika Mazingira Yanayomzunguka.* Wanafunzi walitakiwa kusoma vipengele, kuchagua herufi ya jibu sahihi na kuiandika katika kisanduku kilichoachwa wazi. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 16.

Katika swali hili, mwanafunzi alihesabika kuwa na utendaji hafifu iwapo alishindwa kujibu kipengele hata kimojawapo, au aliweza kujibu vipengele viwili pekee. Mwanafunzi aliyeweza kujibu vipengele vitatu hadi vitano alikuwa na utendaji wa wastani, na mwanafunzi aliyeweza kujibu vipengele sita hadi saba alikuwa na utendaji mzuri. Kwa upande mwingine, mwanafunzi aliyeweza kujibu vipengele vyote vinane alikuwa na utendaji mzuri sana.

Jumla ya wanafunzi 1,560,874 (100%) walijibu swali hili, ambapo wanafunzi 202,160 (13.0%) walikuwa na utendaji mzuri sana. Wanafunzi waliokuwa na utendaji mzuri ni 583,325 (37.3%) kwa kuwa waliweza kujibu kwa usahihi vipengele kati ya sita na saba vya swali hilo.

Kwa upande mwingine, jumla ya wanafunzi 506,561 (32.5%) walikuwa na utendaji wa wastani. Kati yao, wanafunzi 130,724 (8.4%) walijibu kwa usahihi vipengele vitatu, 157,014 (10.1%) walijibu vipengele vinne na wanafunzi 218,823 (14.0%) walijibu vipengele vitano.

Aidha, wanafunzi 268,828 (17.2%) walikuwa na utendaji hafifu, kwa kuwa hawakufaulu swali hilo. Miongoni mwao, 50,671 (3.2%) hawakuweza kujibu kipengele chochote, wengine 94,559 (6.1%) walijibu kwa usahihi kipengele kimoja tu, na wanafunzi 123,598 (7.9%) waliweza kujibu kwa usahihi vipengele viwili. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwani 1,292,046 (82.8%) walipata kuanzia alama 6 hadi 16. Chati Na. 1 inaonesha mchanganuo wa viwango vya ufaulu wa wanafunzi katika swali hili.



Chati Na 1: *Ufaulu wa wanafunzi katika swali la 1*

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi ulifanyika na kubaini mambo mbalimbali katika kila swali kama ifuatavyo:

(i) Kipi kinahusika zaidi na uharibifu wa mazingira katika maeneo ya vijijini?

A Kelele kutoka gereji na karakana

B Moshi wa viwandani

C Hewa chafu kutoka katika magari na mashine

D Uchomaji wa mkaa

Swali hili lilitungwa kutoka kwenye umahiri mahususi wa *Kutunza Mazingira ya Jamii Inayomzunguka.* Kipengele hiki kilipima uwezo wa wanafunzi kubaini chanzo cha uharibifu wa mazingira katika maeneo ya vijijini. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri kwani, wanafunzi wengi walichagua jibu sahihi *D, Uchomaji wa mkaa*. Wanafunzi hao walikuwa na uelewa wa kutosha wa kubainisha vitendo vinavyochangia uharibifu wa mazingira ya kijijini.

Pamoja na wanafunzi wengi kujibu kwa usahihi, wapo waliochagua vipotoshi *A, Kelele kutoka gereji na karakana*, *B, Moshi wa viwandani* na *C*, *Hewa chafu kutoka katika magari na mashine*. Wanafunzi hao walikosa maarifa ya kubainisha vitendo vinavyochangia uharibifu wa mazingira kati ya vijijini na mijini. Tofauti ya uharibifu wa mazingira kati ya maeneo ya vijijini na mijini inahusiana na aina ya shughuli za kiuchumi zinazofanywa katika maeneo hayo. Wanafunzi hao walishindwa kuelewa kuwa vyanzo vitatu vya uharibifu wa mazingira vilivyooneshwa katika vipotoshi vimeshamiri maeneo ya mijini na sio vijijini. Shughuli zinazofanyika katika gereji, karakana na viwandani zinafanyika zaidi maeneo ya mijini.

(ii) Vipi miongoni mwa vitu vifuatavyo vinawakilisha sehemu ya mazingira ya mjini?

A Mapori, mashamba na wanyama

B Maduka makubwa, viwanja vya ndege na hospitali

C Mashamba makubwa, mapori na wanyama

D Mapori, mashamba na maduka makubwa

Swali hili lilitungwa kutoka kwenye umahiri mahususi wa *Kutunza Mazingira ya Jamii* inayomzunguka. Swali lilipima uwezo wa mwanafunzi wa kubaini vitu vinavyowakilisha mazingira ya mijini. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa kiwango kizuri, kwani wanafunzi wengi waliweza kuchagua jibu sahihi *B, Maduka makubwa, viwanja vya ndege na hospitali*. Wanafunzi hao wanatambua namna ambavyo maeneo ya mijini yana wakazi wengi, ambapo huduma bora za biashara, usafiri na matibabu huhitajika kutokana na wingi wa watu katika maeneo hayo.

Hata hivyo, wanafunzi wengine walichagua vipotoshi *A, Mapori*, *mashamba na wanyama*, *C, mashamba makubwa, mapori na wanyama,* na *D, Mapori, mashamba na maduka makubwa.* Vipotoshi hivi vilichaguliwa na wanafunzi waliokosa maarifa juu ya mazingira ya mijini. Wanafunzi hao walishindwa kutofautisha vitu vinavyopatikana kati ya maeneo ya vijijini na mijini ambavyo vinahusiana na shughuli za kiuchumi katika maeneo hayo. Wanafunzi hao, walipaswa kuelewa kwamba idadi kubwa ya watu waishio maeneo ya mijini wanahitaji vitu kama maduka makubwa, usafiri na hospitali ili kuweza kutoa huduma ya kujitosheleza kulingana na mahitaji yao.

(iii) Yapi ni matumizi ya Mbao?

A Kuchoma mkaa

B Kutengeneza kamba

C Kutengeneza samani

D Kutengeneza magari

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri mahususi wa *Kutunza Mazingira ya Jamii Inayomzunguka.* Swali lilipima uwezo wa mwanafunzi kubaini vifaa mbalimbali vinavyotokana na mbao. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa mzuri, kwa kuwa wanafunzi wengi waliweza kuchagua jibu sahihi *C, Kutengeneza samani*. Wanafunzi hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu matumizi ya mbao. Pia wanafunzi wengi wana uelewa wa samani ambazo hutengenezwa kwa mbao; mfano viti, meza, madawati na makabati.

Wanafunzi wengine walishindwa kuchagua jibu sahihi, na hivyo kuchagua kipotoshi; *A, Kuchoma mkaa.* Wanafunzi hao walishindwa kuelewa kuwa mkaa hutengenezwa na magogo ya miti siyo mbao. Baadhi ya wanafunzi waliochagua kipotoshi *B, Kutengeneza kamba.* Wanafunzi hawa pia walikosa maarifa ya kubaini kuwa kamba hutengenezwa kwa kutumia nyuzi za katani na sio mbao. Wanafunzi wengine walichagua kipotoshi *D, Kutengeneza magari*. Wanafunzi hao hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu vifaa vinavyotumika kutengenezea magari. Wanafunzi hao walipaswa kuelewa kuwa magari kwa kiwango kikubwa hutengenezwa kwa kutumia vyuma na sio mbao.

(iv) Hewa inayosafiri hujulikana kama:

A Upepo

B Maji

C Jotoridi

D Mawingu

Swali hili limetoka kwenye umahiri mahususi wa *Kutumia Elimu ya Hali ya Hewa katika Shughuli za kila Siku*. Swali lilipima uwezo wa wanafunzi kufafanua dhana ya hali ya hewa. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa ni wa kiwango kizuri, kwani wanafunzi wengi waliweza kuchagua jibu sahihi *A, Upepo.* Uchaguzi wa jibu sahihi unatokana na maarifa waliyokuwa nayo juu ya dhana ya hali ya hewa na vipengele vyake.

Kwa upande mwingine, baadhi ya wanafunzi walichagua kipotoshi *B, Maji*. Wanafunzi hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu vipengele vya hali ya hewa, kwani walishindwa kubaini kuwa maji si kepengele cha hali ya hewa. Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi walichagua kipotoshi *C, Jotoridi* na weningine kipotoshi *D, Mawingu*. Vipotoshi hivi ni miongoni mwa vipengele vya hali ya hewa, lakini sio hewa inayosafiri. Wanafunzi hao pia hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya tabia ya vipengele vya hali ya hewa.

(v) Mazingira yamegawanyika katika makundi makuu mawili ambayo ni:

A Vitu hai na mimea

B Vitu visivyo hai na wanyama

C Vitu hai na visivyo hai

D Mimea na wanyama

Swali hili lilitungwa kutoka kwenye umahiri mahususi wa *Kutunza Mazingira ya Jamii Inayomzunguka*. Swali lilipima uwezo wa mwanafunzi kufafanua dhana ya mazingira. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa ni wa kiwango kizuri, kwani wanafunzi wengi waliweza kuchagua jibu sahihi *C, vitu hai na* visivyo *hai.* Uchaguzi huo unadhihirisha ujuzi na maarifa ya kutosha waliyonayo wanafunzi katika kuelewa vitu vinavyounda mazingira.

Hata hivyo wanafunzi wengine walichagua kipotoshi *A, Vitu hai na mimea*. Wanafunzi hao walishindwa kuelewa kuwa vitu hai na mimea ni vitu viwili visivyotenganishwa. Hii ni kwa sababu mimea ni sehemu ya vitu hai, hivyo kwa namna moja au nyingine ni kitu kimoja. Inapaswa ieleweke kwamba, mazingira yanaundwa na vitu hai na visivyo hai.

Wanafunzi wengine walichagua kipotoshi B, *Vitu visivyo hai na wanyama*. Wanafunzi hawa walipaswa kuelewa kuwa mazingira yanaundwa na vitu hai na visivyo hai. Vitu hai vinajumuisha mimea na wanyama, na sio wanyama peke yake kama ilivyo kwenye kipotoshi B. Kwa upande mwingine, wanafunzi waliochagua kipotoshi D, *Mimea na wanyama,* walishindwa kuelewa kuwa mimea na wanyama ni vitu hai ambavyo vinaunda kundi moja la mazingira linaloitwa vitu hai. Wanafunzi hao walipaswa kuelewa kuwa mazingira kwa ujumla yanaundwa na vitu hai pamoja na visivyo hai.

(vi) Ipi ni kazi kuu ya majumba ya makumbusho?

A Kuhifadhi wageni kutoka nje ya nchi

B Kutangaza taarifa za kihistoria

C Kuhifadhi kumbukumbu za kihistoria

D Kuhifadhi mapambo

Swali hili limetungwa kutoka kwenye umahiri mahususi wa *Kutunza Kumbukumbu za Matukio ya Kihistoria*. Swali lilipima maarifa ya wanafunzi katika kubaini kazi za majumba ya makumbusho. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa ni wa kiwango kizuri kwani, wanafunzi wengi waliweza kuchagua jibu sahihi C*, Kuhifadhi kumbukumbu za kihistoria*. Uchaguzi wa jibu hili unaashiria kuwa wanafunzi hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu njia zinazotumika kukusanya na kutunza taarifa za kihistoria, hasa majumba ya makumbusho. Wanafunzi hao walikuwa na uelewa kwamba majumba ya makumbusho ni maeneo ambayo matukio ya zamani ya kihistoria huhifadhiwa. Vitu vingi vinavyowakilisha matukio ya zamani ya kiutamaduni na kimaendeleo huhifadhiwa katika majumba ya makumbusho. Majumba ya makumbusho yanapatikana kuanzia ngazi ya Taifa, mkoa, wilaya hadi kijiji. Baadhi ya majumba ya makumbusho yanayopatikana Tanzania ni Makumbusho ya Taifa yaliyopo Dar es Salaam, Makumbusho ya Mwalimu Julius Nyerere yaliyopo Butiama na Makumbusho ya Azimio la Arusha yaliyopo Arusha.

Baadhi ya wanafunzi walichagua kipotoshi; *A, Kuhifadhi wageni kutoka nje ya nchi.* Wanafunzi hao walihusianisha na kitendo cha wageni kutembelea majumba hayo kwani ni sehemu za vivutio vya utalii. Hivyo, walidhani kuwa majumba ya makumbusho huifadhi wageni hao. Wanafunzi wengine walichagua kipotoshi *B, Kutangaza taarifa za kihistoria.* Wanafunzi hao walishindwa kuelewa kuwa kazi kuu ya majumba ya makumbusho ni kuhifadhi kumbukumbu za kihistoria, na sio kuzitangaza. Wanafunzi waliochagua kipotoshi hicho uenda waliona wageni wakipiga picha katika majumba hayo, hivyo kuhusianisha na utangazaji wa taarifa za kihistoria. Kutangaza taarifa za kihistoria si kazi kuu ya majumba ya makumbusho kwani

si miongoni mwa vyombo vya habari. Kwa upande mwingine, wanafunzi waliochagua kipotoshi *D, Kuhifadhi mapambo,* walihusianisha uwepo wa vifaa vya kale, kama mapambo ya kale na kazi kuu ya majumba ya makumbusho ambayo ni kuhifadhi kumbukumbu za kihistoria. Kwa ujumla, wanafunzi hao walikosa maarifa kuhusu njia zinazotumika kutunza kumbukumbu za matukio ya kihistoria.

(vii) Kwa nini mazingira machafu ni mabaya kwa afya?

A Husababisha ulemavu

B Husababisha uzembe

C Husababisha umasikini

D Husababisha magonjwa

Swali hili lilitoka katika umahiri mahususi wa *Kutunza Mazingira ya Jamii Inayomzunguka*. Swali lilipima uwezo wa wanafunzi kubaini madhara ya kiafya yanayotokana na mazingira machafu. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa ni wa kiwango kizuri kwani, wanafunzi wengi waliweza kuchagua jibu sahihi D*, Husababisha magonjwa*. Wanafunzi hao walikuwa na maarifa juu ya magonjwa yanayosababishwa na uchafu katika mazingira kama vile kipindupindu na kuhara.

Kwa upande mwingine, wanafunzi wengine walichagua kipotoshi *A, Husababisha ulemavu.* Wanafunzi hawa walikosa maarifa ya kutambua kuwa ulemavu hausababishwi na mazingira machafu, bali ulemavu husababishwa na ajali, magonjwa ya muda mrefu, au mtu kuzaliwa na ulemavu. Pia wanafunzi wengine walichagua kipotoshi B*, Husababisha uzembe.* Wanafunzi hao walioshindwa kutofautisha

kati ya sababu na athari za mazingira machafu. Walitakiwa kutambua kuwa uzembe hupelekea mazingira kuwa machafu.

Wanafunzi wengine walichagua kipotoshi C*, Husababisha umasikini*. Wanafunzi hao hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya dhana ya umasikini kwa kuhusianisha na uchafu wa mazingira. Mara nyingi watu maskini huishi kwenye mazingira duni hivyo baadhi ya wanafunzi walishindwa kutofautisha kati ya mazingira duni na uchafu.

(viii) Kazi ipi ya kibinadamu inasababisha uchafuzi wa hewa?

A Viwanda

B Utalii

C Biashara

D Uvuvi

Swali hili lilitungwa kutoka kwenye umahiri mahususi wa *Kutunza Mazingira ya Jamii* Inayomzunguka. Swali lilipima uwezo wa wanafunzi kubaini shughuli za binadamu zinazoweza kuchangia uchafuzi wa hewa. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa ni wa kiwango kizuri kwani, wanafunzi wengi waliweza kuchagua jibu sahihi *A, Viwanda.* Wanafunzi hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu uchafuzi wa mazingira unaotokana na shughuli za uzalishaji viwandani.

Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi walichagua vipotoshi *B, Utalii, C, Biashara* na *D, Uvuvi.* Wanafunzi hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu madhara ya shughuli mbalimbali za binadamu kwenye mazingira. Shughuli zilizotajwa katika vipotoshi hivyo hazina uhusiano na uchafuzi wa hewa. Kwa mfano, utalii ni kitendo cha kutembelea maeneo maalumu kwa ajili ya kujifunza na kujifurahisha.

Kitendo hiki hakisababishi uchafuzi wa hewa. Vilevile, biashara kama shughuli inayohusisha kununua na kuuza bidhaa na huduma mbalimbali haisababishi uchafuzi wa hewa. Pia, uvuvi kama moja ya shughuli za kiuchumi inayohusisha uvuaji wa samaki kutoka katika vyanzo vya maji kama vile mito, mabwawa, maziwa na bahari, haina uhusiano na uchafuzi wa hewa.

2.1.2 Swali la 2: Kufuata Kanuni za Kiuchumi katika Shughuli za Uzalishaji Mali

Katika swali hili, wanafunzi walitakiwa kujibu kipengele cha (i) hadi cha (vi). Walitakiwa kuoanisha maelezo ya changamoto za shughuli za kiuchumi zilizopo katika **Fungu A.** na aina za shughuli za kiuchumi katika **Fungu B.** Wanafunzi hao, walitakiwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano. Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kufuata Kanuni za Kiuchumi katika Shughuli za Uzalishaji Mali* na umahiri mahususi wa *Kuthamini na Kulinda Rasilimali za Nchi.* Swali hili lilipima maarifa ya wanafunzi katika kubaini changamoto zinazozikabili shughuli mbalimbali za uzalishaji mali. Jumla ya alama kwa swali hili zilikuwa 12.

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 1,560,874 (100%) ambapo wanafunzi 219,177 (14.0%) walipata alama zote 12 ambao ni ufaulu mzuri sana, na wanafunzi 437,745 (28.1%) walipata alama 8 hadi 10 ambao ni ufaulu mzuri. Kwa upande mwingine, wanafunzi 446,151 (28.6%) walipata alama 4 hadi 6 ambao ni ufaulu wa wastani na wanafunzi 457,801 (29.3%) walipata alama 0 hadi 2 ambao ni ufaulu hafifu. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri ukizingatia kuwa wanafunzi 1,103,073 (70.7%) walipata alama 4 hadi 12 kama chati Na. 2 inavyoonesha.



Chati Na. 2: *Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 2*

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika swali hili unaonesha kuwa wanafunzi 219,177 (14.0%) walijibu kwa usahihi vipengele vyote sita na hivyo kupata alama zote 12. Hii inaashiria kuwa wanafunzi hao walikuwa na uelewa mkubwa na maarifa ya kutosha juu ya umahiri mkuu unaohusu *Kufuata Kanuni za Kiuchumi katika Shughuli za Uzalishaji Mali* hasa umahiri mahsusi unaohusu *Kutambua Shughuli za Uzalishaji Mali katika Jamii.* Wanafunzi hao waliweza kuoanisha maelezo ya changamoto za shughuli za kiuchumi, na aina ya shughuli husika. Kielelezo Na 2.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi swali hili.

2. Oanisha changamoto za shughuli za kiuchumi zilizopo katika **Fungu A** na aina ya shughuli za kiuchumi katika **Fungu B** kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano.

	Fungu A	Herufi	Fungu B
(i)	Kukosekana kwa malisho mazuri na ya kutosha.	(E)	A. Kilimo B. Misitu C. Uchimbaji wa madini D. Ufugaji wa ndege E. Ufugaji wa wanyama F. Utalii G. Uvuvi H. Uwindaji
(ii)	Kupungua kwa samaki kutokana na matumizi ya sumu na nyavu zenye matundu madogo.	(G)	
(iii)	Kukosekana kwa teknolojia ya kisasa katika migodi.	(C)	
(iv)	Matangazo duni ya kuvutia wageni kuja kuangalia urithi wa asili na mbuga za wanyama.	(F)	
(v)	Utengenezaji wa mkaa na kukata miti hovyo.	(B)	
(vi)	Kupungua kwa chakula kutokana na upungufu wa mvua na udongo kukosa rutuba.	(A)	

Kielelezo Na. 2.1: *Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu vipengele vyote vya swali la 2 kwa usahihi*

Kwa upande mwingine, wanafunzi 437,745 (28.1%) walimudu kuoanisha vipengele 4 hadi 5. Wanafunzi hawa walielewa baadhi ya shughuli na changamoto zake. Baadhi ya wanafunzi walimudu kuoanisha kwa usahihi vipengele (i), (ii), (iii), (iv), na (vi) vya Fungu A, kwa herufi E, G, C, F, na A kutoka Fungu B mtawalia. Hii inatokana na maarifa waliyokuwa nayo kuhusu shughuli hizo za kiuchumi ambazo zimezoeleka katika mazingira yao. Kwa upande mwingine, wanafunzi wengi walishindwa kuhusianisha kwa usahihi kipengele cha (v) na herufi B *misitu.* Hii ni kwa sababu hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya changamoto zinazokabili misitu. Hii inatokanana na baadhi ya wanafunzi kuishi katika maeneo yasiyo na misitu kama vile baadhi ya maeneo ya mikoa ya katikati mwa Tanzania na maeneo ya mijini. Pia, wanafunzi wengine walishindwa kubaini jibu sahihi kwasababu walihusianisha na maisha yao ya kila siku ambapo mkaa huweza kutengenezwa kwa kutumia miti inayopatikana katika mazingira wanayoishi ambayo si misitu. Kwa nyongeza, wanafunzi wengi waliweza kuhusianisha kipengele (vi) na

herufi “A” kutokana na umaarufu wa shughuli za kilimo katika jamii ya Watanzania. Kielelezo Na 2.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi kipengele cha (v) katika swali hili.

2. Oanisha changamoto za shughuli za kiuchumi zilizopo katika **Fungu A** na aina ya shughuli za kiuchumi katika **Fungu B** kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano.

	Fungu A	Herufi	Fungu B
(i)	Kukosekana kwa malisho mazuri na ya kutosha.	(E)	A. Kilimo B. Misitu C. Uchimbaji wa madini D. Ufugaji wa ndege E. Ufugaji wa wanyama F. Utalii G. Uvuvi H. Uwindaji
(ii)	Kupungua kwa samaki kutokana na matumizi ya sumu na nyavu zenye matundu madogo.	(G)	
(iii)	Kukosekana kwa teknolojia ya kisasa katika migodi.	(C)	
(iv)	Matangazo duni ya kuvutia wageni kuja kuangalia urithi wa asili na mbuga za wanyama.	(F)	
(v)	Utengenezaji wa mkaa na kukata miti hovyo.	(D)	
(vi)	Kupungua kwa chakula kutokana na upungufu wa mvua na udongo kukosa rutuba.	(A)	

Kielelezo Na. 2.2: *Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi kipengele (v) cha swali la 2*

Uchambuzi zaidi wa majibu unaonesha kuwa wanafunzi 446,151 (28.6%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata kati ya alama 4 hadi 6. Wanafunzi wengi walipata alama 6. Hii inaonesha kuwa waliweza kujibu vipengele 3 kati ya 6. Wengi wa wanafunzi hao walijibu kwa usahihi kipengele (i), (iii) na (vi). Wanafunzi walioweza kuhusianisha kwa usahihi kipengele (i) walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya changamoto za ufugaji wa wanyama. Hii ni kwa sababu waliweza kuhusianisha dhana walizojifunza kuhusu ufugaji wa wanyama, na maisha ya kila siku. Shughuli hii ni maarufu Tanzania kwani jamii nyingi zinafuga wanyama kwa idadi tofauti.

Vilevile, wanafunzi walioweza kuoanisha kwa usahihi kipengele (ii) walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu changamaoto inayohusu uvuvi. Hii ni kwasababu uvuvi ni shughuli inayofanywa na jamii nyingi Tanzania kwa sababu ya uwepo wa vyanzo vya maji kama vile mito, mabwawa, maziwa na bahari. Baadhi ya wanafunzi hao walihusianisha changamoto za uvuvi na zile walizoziona kwenye vyombo vya habari zinazohusu uchomaji wa zana za uvuvi zisizotakiwa, hasa nyavu zenye matundu madogo.

Vilevile, vipengele vya (iii) na (iv) havikujibiwa kwa usahihi kutokana na wanafunzi kutokuwa na maarifa ya kutosha juu ya uchimbaji wa madini na utalii. Hii ni kwasababu shughuli hizo sio maarufu kwa baadhi ya maeneo ya Tanzania. Mfano, uchimbaji wa madini umeshamiri katika maeneo yenye rasilimali hiyo, na utalii hufanyika zaidi kwenye maeneo yenye vivutio vya utalii. Kwa hiyo, baadhi ya wanafunzi walishindwa kuhusianisha dhana ya uchimbaji wa madini, na utalii na uhalisia wa shughuli hizo. Kielelezo Na 2.3 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu kwa usahihi vipengele 3 katika swali hili.

2. Oanisha changamoto za shughuli za kiuchumi zilizopo katika **Fungu A** na aina ya shughuli za kiuchumi katika **Fungu B** kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano.

	Fungu A	Herufi	Fungu B
(i)	Kukosekana kwa malisho mazuri na ya kutosha.	(E)	A. Kilimo
(ii)	Kupungua kwa samaki kutokana na matumizi ya sumu na nyavu zenye matundu madogo.	(G)	B. Misitu C. Uchimbaji wa madini D. Ufugaji wa ndege
(iii)	Kukosekana kwa teknolojia ya kisasa katika migodi.	(D)	E. Ufugaji wa wanyama
(iv)	Matangazo duni ya kuvutia wageni kuja kuangalia urithi wa asili na mbuga za wanyama.	(C)	F. Utalii G. Uvuvi H. Uwindaji
(v)	Utengenezaji wa mkaa na kukata miti hovyo.	(F)	
(vi)	Kupungua kwa chakula kutokana na upungufu wa mvua na udongo kukosa rutuba.	(A)	

Kielelezo Na. 2.3: *Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi vipengele (i), (ii) na (vi) vya swali la 2*

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, wanafunzi, 457,801 (29.3%) walikuwa na ufaulu hafifu ambapo kati yao 212,974 (13.6%) walipata sifuri. Wanafunzi 244,827 (15.7%) waliobaki walipata alama 2 kwani waliweza kujibu kwa usahihi kipengele kimoja tu cha swali hili. Kipengele (vi) ndicho kilijibiwa na wanafunzi wengi zaidi kwa sababu changamoto iliyotajwa inahusiana na shughuli kuu ya kiuchumi inayofanyika nchini Tanzania. Kielelezo Na 2.4 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi kipengele kimoja tu cha swali hili.

2. Oanisha changamoto za shughuli za kiuchumi zilizopo katika **Fungu A** na aina ya shughuli za kiuchumi katika **Fungu B** kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano.

	Fungu A	Herufi	Fungu B
(i)	Kukosekana kwa malisho mazuri na ya kutosha.	(H)	A. Kilimo B. Misitu C. Uchimbaji wa madini D. Ufugaji wa ndege E. Ufugaji wa wanyama F. Utalii G. Uvuvi H. Uwindaji
(ii)	Kupungua kwa samaki kutokana na matumizi ya sumu na nyavu zenye matundu madogo.	(C)	
(iii)	Kukosekana kwa teknolojia ya kisasa katika migodi.	(F)	
(iv)	Matangazo duni ya kuvutia wageni kuja kuangalia urithi wa asili na mbuga za wanyama.	(E)	
(v)	Utengenezaji wa mkaa na kukata miti hovyo.	(G)	
(vi)	Kupungua kwa chakula kutokana na upungufu wa mvua na udongo kukosa rutuba.	(A)	

Kielelezo Na. 2.4: *Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi kipengele (vi) tu cha swali la 2*

Aidha, wanafunzi waliopata 0 hawakuwa na maarifa juu ya umahiri mkuu unaohusu *Kufuata Kanuni za Kiuchumi katika Shughuli za Uzalishaji Mali,* hasa umahiri mahususi unaohusu *Kutambua Shughuli za Uzalishaji Mali katika Jamii*. Wanafunzi hao walishindwa kuoanisha shughuli za kiuchumi na maelezo ya changamoto husika. Kielelezo Na 2.5 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu swali hili.

2. Oanisha changamoto za shughuli za kiuchumi zilizopo katika **Fungu A** na aina ya shughuli za kiuchumi katika **Fungu B** kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano.

	Fungu A	Herufi	Fungu B
(i)	Kukosekana kwa malisho mazuri na ya kutosha.	(C)	A. Kilimo B. Misitu C. Uchimbaji wa madini D. Ufugaji wa ndege E. Ufugaji wa wanyama F. Utalii G. Uvuvi H. Uwindaji
(ii)	Kupungua kwa samaki kutokana na matumizi ya sumu na nyavu zenye matundu madogo.	(B)	
(iii)	Kukosekana kwa teknolojia ya kisasa katika migodi.	(E)	
(iv)	Matangazo duni ya kuvutia wageni kuja kuangalia urithi wa asili na mbuga za wanyama.	(A)	
(v)	Utengenezaji wa mkaa na kukata miti hovyo.	(H)	
(vi)	Kupungua kwa chakula kutokana na upungufu wa mvua na udongo kukosa rutuba.	(G)	

Kielelezo Na. 2.5: *Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi vipengele vyote vya swali la 2*

2.2 Sehemu B: Maswali ya Majibu Mafupi

Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili ya majibu mafupi, swali la 3 na 4. Katika swali la 3, wanafunzi walitakiwa kusoma kifungu cha habari, na kisha kujibu maswali yaliyotokana na kifungu hicho. Swali hilo lilikuwa na jumla ya vipengele saba vyenye alama 2 kila kimoja hivyo kufanya jumla ya alama 14. Katika swali la 4, wanafunzi walitakiwa kusoma ramani waliyopewa na kisha kujibu maswali kutokana na alama za ramani hiyo. Swali hilo lilikuwa na vipengele 4. Kila kipengele kilikuwa na alama 2, hivyo kufanya swali kuwa na jumla ya alama 8. Uchambuzi wa majibu unaonesha kuwa, ufaulu katika swali la 3 ulikuwa hafifu, na wa wastani katika swali la 4.

2.2.1 Swali la 3: Kutambua Msingi ya Uzalendo katika Jamii.

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu: *Kutambua Misingi ya Uzalendo katika Jamii* na umahiri mahususi *Kudumisha Utamaduni wa Mtanzania.* Katika swali hili, wanafunzi walitakiwa kusoma habari kuhusu mfumo wa kwanza wa kiuchumi unaojulikana kama ujima.

Pia, waanafunzi walitakiwa kujibu vipengele vilivyoulizwa kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi zilizoachwa wazi.

Swali hili lilikuwa na vipengele saba yaani (i) hadi (vii). Kipengele cha (i) kilipima ufahamu wa wanafunzi kutambua njia kuu za uzalishaji mali wakati wa ujima. Kipengele cha (ii) kilipima uwezo wa wanafunzi kubaini vifaa vilivyotumika kwa uwindaji katika kipindi hicho. Kipengele cha (iii) kilipima uwezo wa wanafunzi kutambua sababu za kutokuwepo kwa unyonyaji katika mfumo huu wa uzalishaji mali, na kipengele cha (iv) kililenga kupima uwezo wa wanafunzi kubainisha sababu za kutokuwepo kwa biashara katika kipindi hicho. Aidha, kipengele cha (v) kilipima uwezo wa wanafunzi kubainisha wanufaika wa mali zilizozalishwa katika mfumo huu wa uzalishaji mali. Kipengele cha (vi) kilipima uwezo wa wanafunzi kubaini sababu za kutokuwepo kwa ziada iliyozalishwa katika mfumo huu wa uzalishaji mali. Mwisho, kipengele cha (vii) kilipima ufahamu wa wanafunzi kutambua jinsi njia kuu za uzalishaji mali zilivyomilikiwa wakati wa ujima. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 14. Kielelezo Na 3.1 kinaonesha habari iliyotumika katika swali la 3.

3. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.

Ujima ulikuwa mfumo wa kwanza wa kiuchumi ambao binadamu wote waliupitia. Hapakuwa na unyonyaji miongoni mwa watu kwa kuwa kila mmoja alishiriki katika uzalishaji. Katika mfumo huu njia kuu za uzalishaji mali zilikuwa ni ardhi, misitu, maziwa na mito. Wakati wa ujima uzalishaji mali ulikuwa mdogo sana. Hii ilitokana na vitendea kazi duni vilivyotumika. Vilevile hapakuwa na biashara wala kubadilishana bidhaa baina ya watu katika jamii. Hii ilitokana na kukosekana kwa ziada wakati wa kuzalisha. Mfano wa vitendea kazi vilivyotumika ni majembe ya mkono na mishale. Katika kipindi cha ujima, njia za uzalishaji mali na vitendea kazi vilimilikiwa na jamii nzima.

Kielelezo Na. 3.1: *Kifungu cha habari ambacho wanafunzi walitakiwa kusoma na kisha kujibu swali la 3*

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 1,560,874 (100%). Kati ya hao, wanafunzi 17,925 (1.1%) walipata alama zote 14 ambao ni ufaulu mzuri sana, na wanafunzi 112,012 (7.2%) walipata alama kati ya 10 hadi 12 ambao ni ufaulu mzuri. Kwa upande mwingine, wanafunzi 315,365 (20.2%) walipata alama kati ya 6 hadi 8 ambao ni ufaulu wa wastani, na wanafunzi 1,115,572 (71.5%) walipata kati ya 0 hadi alama 4 ambao ni ufaulu hafifu. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa hafifu kwa kuwa ni wanafunzi 445,302 (28.5%) tu walipata kati ya alama 6 hadi 14. Chati Na. 3 inaonesha kiwango cha ufaulu wa wanafunzi katika swali la 3.



Chati Na. 3: *Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 3*

Uchambuzi wa umahiri wa wanafunzi unaonesha kuwa kulikuwa na tofauti kubwa ya alama. Ni wanafunzi 445,302 (28.5%) pekee ndio waliopata alama 6 hadi 14, wakati wanafunzi 1,115,572 (71.5%) walipata 0 hadi alama 4. Wanafunzi waliopata alama zote 14 walikuwa na maarifa ya kutosha kwani walijibu vipengele vyote 7 kwa usahihi. Wanafunzi waliopata alama 10 hadi 12 walikuwa katika kiwango kizuri cha ufaulu kwa sababu walijibu kwa usahihi vipengele 5 hadi 6 kati ya 7.

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliopata alama kati ya 6 hadi 8 walikuwa kwenye kiwango cha wastani cha ufaulu kwa sababu waliweza kujibu kwa usahihi vipengele 3 hadi 4 kati ya 7. Hata hivyo, wanafunzi waliopata alama 0 hadi 4 walikuwa kwenye kiwango hafifu cha ufaulu. Wanafunzi hao, walishindwa kujibu kipengele chochote au waliweza kujibu kwa usahihi kipengele 1 au 2 kati ya vipengele 7.

Katika kipengele cha (i), baadhi ya wanafunzi waliweza kubaini kwa ufasaha njia kuu za uzalishaji mali wakati wa ujima kuwa ni *Ardhi, Misitu, Maziwa na Mito*. Jibu hili ni kiashiria kuwa wanafunzi hao walikuwa na umahiri wa kutosha kusoma habari na kubaini ujumbe mahususi uliokuwemo katika habari hiyo.

Kipengele cha (ii) kilipima uwezo wa wanafunzi kubaini aina ya kifaa kilichotumika katika uwindaji kipindi cha ujima. Ufaulu katika kipengele hiki ulikuwa wa kiwango kizuri. Wanafunzi wengi waliweza kubaini kuwa *mishale* ndiyo kifaa kilichotumika katika uwindaji kipindi cha ujima. Hii inamaanisha kuwa, wanafunzi hao walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya zana za uzalishaji mali zilizotumika wakati wa ujima. Vilevile, baadhi ya wanafunzi hao walihusianisha swali hili na maisha yao ya kila siku kwa kuwa baadhi ya zana hizo bado zinatumika katika jamii za Kitanzania kwa shughuli sawa na hizo.

Katika kipengele cha (iii), wanafunzi walitakiwa kubaini sababu za kutokuwepo kwa unyonyaji katika mfumo wa ujima. Ufaulu wa wanafunzi katika kipengele hiki ulikuwa ni wa kiwango cha wastani. Wanafunzi waliokuwa na uelewa wa kutosha juu ya uhusiano miongoni mwa wanajamii katika kipindi cha ujimama waliweza kubaini sababu za kutokuwepo kwa unyonyaji katika mfumo huu wa

uzalishaji kuwa *kila mmoja alishiriki katika uzalishaji mali*. Jibu hili ni kiashiria kuwa wanafunzi hao walikuwa na maarifa ya kutosha katika kusoma na kuelewa habari ipasavyo. Pia, walikuwa na maarifa juu ya namna watu walivyofanya kazi kwa pamoja, na kugawana sawa kile kilichopatikana wakati wa ujima.

Katika kipengele cha (iv), wanafunzi walitakiwa kubaini sababu za kutokuwa na biashara katika mfumo wa ujima. Ufaulu katika kipengele hiki ulikuwa hafifu, japokuwa baadhi ya wanafunzi waliweza kubaini kuwa katika kipindi cha ujima hapakuwa na biashara kutokana na *kukosekana kwa ziada katika uzalishaji mali*. Jibu hili ni kiashiria kuwa wanafunzi hao walikuwa na umahiri wa kutosha katika kusoma na kujibu maswali yatokanayo na kifungu cha habari. Vilevile, wanafunzi hao walikuwa na uelewa kuwa, ili biashara ifanyike lazima kuwe na ziada katika uzalishaji.

Kipengele cha (v) kiliwataka wanafunzi kubaini aliyefaidika na mali zilizozalishwa katika mfumo wa ujima. Ufaulu katika kipengele hiki ulikuwa wa wastani kwani baadhi ya wanafunzi waliweza kubainisha kwa usahihi kuwa *Jamii nzima/wanajamii/kila mwanajamii* alifaidika na mali iliyozalishwa katika mfumo huu wa uzalishaji mali. Hii ni kutokana na ushiriki wa jamii nzima katika uzalishaji. Jibu hili lilionesha kuwa wanafunzi hao walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya uhusiano baina ya wanajamii wakati wa ujima. Wanafunzi hao, waliweza kubaini kuwa uhusiano uliokuwepo wakati wa ujima ulikuwa ni uhusiano wa kindugu, ambapo kila mwanajamii alishiriki katika uzalishaji mali. Kwa sababu hiyo, njia kuu za uzalishaji mali na mazao viligawanywa sawa kwa kila mwanajamii kulingana na mahitaji yao.

Kipengele cha (vi) kilipima uwezo wa wanafunzi kubaini sababu zakutokuwepo kwa mazao ya ziada yaliyozalishwa katika ujima. Kiwango cha ufaulu kwa kipengele hiki kilikuwa hafifu, kwani baadhi ya wanafunzi waliweza kuandika jibu sahihi *vitendea kazi duni*. Wanafunzi hao walikuwa na maarifa kuwa wakati wa ujima kulikuwa na teknolojia duni iliyopelekea uzalishaji wa kukidhi mahitaji yao tu na sio kubadilishana. Jibu hili linaashiria kuwa wanafunzi hao waliweza kuhusianisha swali hilo na maisha ya kila siku, kwamba teknolojia ya kisasa hupelekea zana zilizo bora kama vile treka, mashine zakupanda na kuvuna mazao. Zana hizi za kisasa hutumika katika shughuli mbalimbali za kiuchumi hasa kilimo, nahuchochea uzalishaji wa ziada.

Kipengele cha (vii) kilipima uwezo wa wanafunzi kubaini jinsi njia za uzalishaji mali zilivyomilikiwa wakati wa ujima. Kiwango cha ufaulu wa wanafunzi katika kipengele hiki kilikuwa hafifu kwani wanafunzi wachache waliweza kueleza namna ambavyo njia za uzalishaji mali zilimilikiwa na *jamii nzima* wakati wa ujima. Wanafunzi hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuwa katika mfumo wa ujima, njia kuu za uzalishaji mali zilimilikiwa na jamii husika kwa ujumla. Kielelezo Na. 3.2 kinaonesha mfano wa majibu mazuri ya swali la 3 ya mwanafunzi mmojawapo.



(i) Bainisha njia mojawapo kuu ya uzalishaji mali wakati wa ujima.
Ardhi, misitu, maziwa na mito

(ii) Kifaa gani kilitumika katika kuwinda? Mishale

(iii) Kwa nini hapakuwa na unyonyaji katika mfumo huu wa uzalishaji mali?
Kwa kuwa kilammoja alishiriki katika uzalishaji mali

(iv) Kwa nini hapakuwa na biashara katika mfumo huu wa uzalishaji mali?
ilitokana na ukosefu wa ziada wa kuzalisha

(v) Nani alifaidika kutokana na mali zilizozalishwa katika mfumo huu wa uzalishaji mali? Jamii nzima

(vi) Kwa nini hapakuwa na mazao ya ziada yaliyozalishwa katika mfumo huu wa uzalishaji mali? Kulikuwa na vitendaku kazi dum

(vii) Ni kwa jinsi gani njia za uzalishaji mali zilimilikiwa?
Zilimilikiwa na jamii nzima

Kielelezo Na. 3.2: *Sampuli ya majibu sahihi ya swali la 3*

Kwa nyongeza, uchambuzi ulibaini kuwa baadhi ya wanafunzi walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kati ya 6 hadi 8, ikiwa ni sawa na kujibu kwa usahihi vipengele 3 hadi 4 kati ya vipengele 7. Kufaulu huku kwa wastani kulisababishwa na kukosa ujuzi wa kutosha katika kusoma habari kwa kina. Jambo hili lilisababisha wanafunzi kujibu kwa usahihi vipengele vichache. Mfano, baadhi ya wanafunzi walijibu vizuri kipengele cha (i), (ii), (iii) na (v), na kukosa vipengele vilivyobaki. Kielelezo Na. 3.3 kinaonesha mfano wa majibu ya wastani kutoka kwa mwanafunzi mmojawapo.



(i) Bainisha njia mojawapo kuu ya uzalishaji mali wakati wa ujima.
ardhi misitu maziwa pamito

(ii) Kifaa gani kilitumika katika kuwinda? mshale

(iii) Kwa nini hapakuwa na unyonyaji katika mfumo huu wa uzalishaji mali?
kwasababu kila mmoja alishiriki katika uzalishaji

(iv) Kwa nini hapakuwa na biashara katika mfumo huu wa uzalishaji mali?
kwasababu uzalishaji mali ulikua mdogo sana

(v) Nani alifaidika kutokana na mali zilizozalishwa katika mfumo huu wa uzalishaji mali? Jamii nzima

(vi) Kwa nini hapakuwa na mazao ya ziada yaliyozalishwa katika mfumo huu wa uzalishaji mali? kwasababu palikuwa hamna biashara

(vii) Ni kwa jinsi gani njia za uzalishaji mali zilimilikiwa?
Njia za uzalishaji mali ni zitenzeci kazi

Kielelezo 3.3: *Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyepata ufaulu wa wastani*

Pia, uchambuzi unaonesha kuwa baadhi ya wanafunzi walipata kati ya 0 hadi alama 4. Hali hii inaashiria kuwa wanafunzi hao hawakuelewa kikamilifu matakwa ya swali, hivyo kujibu kwa usahihi vipengele visivyosizidi 2 kati ya vipengele 7 vya swali hilo. Vilevile, wanafunzi wengine katika kundi hilo hawakuwa na stadi za kutosha juu ya kusoma na kuelewa habari, hivyo kutoweza kujibu kipengele chochote cha swali hilo, na kupata sifuri. Vielelezo Na. 3.4 na 3.5 vinaonesha sampuli ya majibu hafifu ya wanafunzi katika swali la 3.



(i) Bainisha njia mojawapo kuu ya uzalishaji mali wakati wa ujima.
alizi, misitu, maziwa, nafto

(ii) Kifaa gani kilitumika katika kuwinda? manati

(iii) Kwa nini hapakuwa na unyonyaji katika mfumo huu wa uzalishaji mali?
Majengo yamboa na mishale

(iv) Kwa nini hapakuwa na biashara katika mfumo huu wa uzalishaji mali?
asidi, misitu, maziwa, nafto

(v) Nani alifaidika kutokana na mali zilizozalishwa katika mfumo huu wa uzalishaji mali? Vitendea ~~na~~ kazi duania

(vi) Kwa nini hapakuwa na mazao ya ziada yaliyozalishwa katika mfumo huu wa uzalishaji mali? hapakuwa na biashara wala kubadilishana

(vii) Ni kwa jinsi gani njia za uzalishaji mali zilimilikiwa?
ujima na mfumo wa kwanza

Kielelezo Na. 3.4: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi mwenye ufaulu hafifu aliyejibu kwa usahihi kipengele cha (i) tu cha swali la 3



(i) Bainisha njia mojawapo kuu ya uzalishaji mali wakati wa ujima.
Hapakuwa na unyonyaji

(ii) Kifaa gani kilitumika katika kuwinda? mage mishale

(iii) Kwa nini hapakuwa na unyonyaji katika mfumo huu wa uzalishaji mali?
hapakuwa na biashara wala kubadilishana bidhaa

(iv) Kwa nini hapakuwa na biashara katika mfumo huu wa uzalishaji mali?
Ujima ulikuwa ni mfumo wakwanza

(v) Nani alifaidika kutokana na mali zilizozalishwa katika mfumo huu wa uzalishaji mali? watu wengi

(vi) Kwa nini hapakuwa na mazao ya ziada yaliyozalishwa katika mfumo huu wa uzalishaji mali? watu wengi hawakupanda

(vii) Ni kwa jinsi gani njia za uzalishaji mali zilimilikiwa?
Kuliko kukuza unyonyaji

Kielelezo Na. 3.5: *Sampuli ya majibu ya mwanafunzi mwenye ufaulu hafifu aliyejibu kwa usahihi kipengele cha (ii) tu cha swali la 3*

Uchambuzi zaidi wa viwango vya umahiri kwa kila kipengele katika swali la 3 unaonesha tofauti ya majibu, jambo lililochangia tofauti mkubwa kwenye ufaulu. Tofauti ilikuwa ndogo katika kipengele cha

(i) na (ii), wastani katika kipengele cha (iii) na (v), na kubwa katika vipengele cha (iv), (vi) and (vii).

Katika kipengele cha (i), ufaulu ulikuwa mzuri. Wanafunzi wengi waliandika jibu sahihi. Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi waliandika majibu yasiyo sahihi kama vile *ulikuwa mfumo wa kwanza wa kiuchumi ambao binadamu wote waliupitia, njia kuu za uzalishaji mali zilikuwa chache, nguvukazi ilimilikiwa na jamii nzima* na *zana duni za kufanyia kazi.* Baadhi ya sentensi za majibu haya, zilinakiliwa kutoka kwenye kifungu cha habari. Sentensi hizi haziendani na majibu sahihi. Kwa nyongeza, baadhi ya wanafunzi waliandika dhana ya ujima, badala ya kubainisha njia za uzalishaji mali zilizooneshwa katika habari. Majibu haya yanaonesha kwamba wanafunzi hao hawakuwa na stadi za kusoma na kuelewa maudhui ya habari.

Vilevile, katika kipengele cha (ii) ufaulu wa wanafunzi ulikuwa mzuri. Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi waliandika majibu yasiyo sahihi kama vile *jembe la mkono, manati na mikuki.* Majibu haya yanaashiria kwamba wanafunzi hao hawakuwa na uelewa wa maudhui ya habari. Hivyo, waliandika majibu kutokana na uzoefu wa maisha yao ya kila siku. Mfano, baadhi ya wanafunzi wanaoishi maeneo ya vijijini hutumia manati katika uwindaji wa ndege.

Katika kipengele cha (iii) baadhi ya wanafunzi walijibu kwa kuandika majibu kama vile *kwa sababu hapakuwa na biashara na kubadilishana bidhaa, ilikuwa hatua ya kwanza ya mabadiliko ya mwanadamu,* na *kwa sababu njia kuu za uzalishaji mali hulimilikiwa na jamii nzima.* Majibu haya yanaashiria kuwa wanafunzi hawa

hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya uhusiano kati ya wanajamii wakati wa ujima.

Katika kipengele cha (iv), wanafunzi wengi walishindwa kuandika jibu sahihi. Waliandika majibu tofauti kama vile *kubadilishana bidhaa miongoni mwa watu katika jamii, ongezeko la uzalishaji mali, na ilikuwa mfumo wa kwanza wa kiuchumi.* Majibu hayo yanaashiria kwamba wanafunzi hao hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya chimbuko, na maendeleo ya biashara. Walitakiwa kuelewa kwamba, biashara ilianza baada ya jamii kuanza kuzalisha ziada. Ilikuwa ni kipindi ambacho biashara ya kubadilishana bidhaa ilianza.

Wanafunzi walioshindwa kipengele cha (v) waliandika majibu kama vile, *kwa sababu ya kutumia zana duni, katika kipindi cha ujima, na ambao binadamu* wote *waliupitia*. Haya sio majibu sahihi, bali ni sentensi au maneno yaliyomo katika habari. Majibu haya yanaashiria kuwa wanafunzi hawa hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya namna ya kuhusianisha dhana na matukio ya kihistoria. Walipaswa kuelewa kwamba hakukuwa na matabaka baina ya wanajamii katika kipindi cha ujima. Hivyo, wanajamii wote walifaidika na uzalishaji, na sio, kwa mtu mmoja mmoja.

Katika kipengele cha (vi), baadhi ya wanafunzi walishindwa kuandika jibu sahihi, na kuandika majibu kama vile *kukosekana kwa ziada, kwa sababu hapakuwa na biashara wala kubadilishana bidhaa baina ya watu katika jamii, mifano ya zana zilizotumika zilikuwa ni jembe la mikono na mishale*. Majibu hayo yanaonesha kwamba wanafunzi hao hawakuelewa matakwa ya swali, hivyo walinakili baadhi ya maneno au sentensi kutoka katika kifungu cha habari na kuziandika kama majibu sahihi. Baadhi yao waliandika

sentensi zinazofanana na majibu sahihi, lakini siyo majibu sahihi kwa kipengele cha (vi). Mfano, baadhi ya wanafunzi walitaja majembe ya mkono na mishale ambayo ni mifano ya zana duni. Wanafunzi hao walitaja mifano ya zana duni badala ya kutaja sababu zilizochangia kukosekana kwa ziada wakati wa ujima.

Vilevile, katika kipengele cha (vii), baadhi ya wanafunzi walishindwa kuandika jibu sahihi, hivyo kuandika majibu kama *ulimilikiwa kwa kushiriki katika uzalishaji, njia za uzalishaji zilikuwa chache, ujima, zana za uzalishaji mali zilimilikiwa na jamii nzima,* na *njia kuu za uzalishaji mali zilikuwa ni ardhi, misitu, maziwa na mito.* Majibu haya yanaashiria kwamba wanafunzi hao hawakuelewa matakwa ya swali, hivyo walinakili baadhi ya maneno au sentensi kutoka katika kifungu cha habari.

Kwa upande mwingine, baadhi ya wanafunzi walipata ufaulu hafifu katika kipengele hiki kwani walishindwa kubaini namna njia za uzalishaji mali zilivyomilikiwa wakati wa ujima. Wanafunzi hao hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya tabia za ujima, ambapo moja ya tabia zake ni *wanajamii kumiliki kwa pamoja njia kuu za uzalishaji mali*. Wanafunzi hao walipaswa kuelewa kuwa njia kuu za uzalishaji mali zilimilikiwa na jamii nzima. Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi waliandika ardhi, misitu, maziwa na mito. Wanafunzi hao walitaja njia kuu za uzalishaji mali wakati wa ujima, badala ya kuonesha namna njia hizo zilivyomilikiwa.

2.2.2 Swali la 4: Kutumia Ramani na Elimu ya Anga katika Maisha ya kila Siku

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri mkuu wa *Kutumia Ramani na Elimu ya Anga katika Maisha ya Kila Siku,* na umahiri mahususi

wa *wa Kutumia Ramani katika Mazingira Mbalimbali.* Katika swali hili, wanafunzi walitakiwa kusoma ramani waliyopewa ya kijiji cha Lumbila, kisha wajibu maswali kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi zilizoachwa wazi. Swali hili lilikuwa na vipengele vinne; (i), (ii), (iii) na (iv).

Kipengele cha (i) kilipima uwezo wa wanafunzi katika kubaini alama inayowakilisha shule, na kutaja idadi ya shule zilizoonekana kwenye ramani hiyo. Kipengele cha (ii) kilipima uwezo wa wanafunzi katika kubaini mambo mawili; moja ni alama inayowakilisha kanisa na kisha kubaini pande kuu nne za Dunia kwa kuelezea upande ambao kanisa linapatikana. Kipengele cha (iii) kilipima uwezo wa wanafunzi katika kubaini alama inayowakilisha milima na idadi yake, na kipengele cha (iv) kilipima uwezo wa wanafunzi katika kubaini alama inayowakilisha barabara, na kubainisha idadi za barabara zinazoelekea Kaskazini mwa kijiji. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 8. Kielelezo Na. 4.1 kinaonesha ramani ya kijiji cha Lumbila iliyotumika katika swali la 4.



Kielelezo Na. 4.1: *Ramani ya kijiji cha Lumbila iliyotumika katika swali la 4*

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 1,560,874 (100%). Wanafunzi 96,108 (6.2%) kati ya hao walipata alama zote 8 ambao ni ufaulu mzuri sana, na wanafunzi 225,154 (14.4%) walipata alama 6 ambao ni ufaulu mzuri. Kwa upande mwingine, wanafunzi 299,040 (19.1%) walipata alama 4 ambao ni ufaulu wa wastani, na wanafunzi 940,572 (60.3%) walipata 0 hadi alama 2 ambao ni ufaulu hafifu. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa ni wa wastani kwani wanafunzi 620,302 (39.7%) walipata kati ya alama 4 hadi 8. Chati Na. 4 inaonesha kiwango cha ufaulu katika swali la 4.



Chati Na.4: *Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 4*

Uchambuzi wa kiwango cha ufaulu katika swali hili ulibaini kuwa, wanafunzi waliopata alama 8 waliweza kujibu vipengele vyote vinne vya swali hili kwa usahihi. Wanafunzi waliopata alama 6 waliweza kujibu kwa usahihi vipengele 3 kati ya vipengele 4. Kwa upande mwingine, wanafunzi waliopata alama 4 waliweza kujibu kwa usahihi vipengele 2 kati ya 4, na wanafunzi waliopata 0 hadi alama 2 aidha, hawakuweza kujibu kwa usahihi kipengele chochote cha swali hilo au waliweza kujibu kwa usahihi kipengele 1 kati ya vipengele 4 vilivyotolewa.

Swali hili lilipima umahiri wa wanafunzi katika kusoma na kutafsiri alama za ramani. Wanafunzi waliopata alama 8 walikuwa na umahiri wa kutosha katika kusoma na kutafsiri alama za ramani. Katika kipengele cha (i), wanafunzi waliokuwa na maarifa ya kutosha waliweza kutoa jibu sahihi. Hii ni kutokana na kuwa na maarifa ya kutosha juu ya usomaji wa ramani. Katika kipengele cha (ii), wanafunzi ambao waliweza kujibu kwa usahihi kipengele hiki waliweza kubaini alama zinazowakilisha *Kanisa* na daraja, na kutoa upande wa kanisa kutoka kwenye daraja ambao ni upande wa *Kusini*. Wanafunzi hao walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya usomaji wa dira, au pande kuu za Dunia. Katika kipengele cha (iii), wanafunzi waliojibu kwa usahihi waliweza kubaini alama inayowakilisha mlima, na kutaja idadi ya milima iliyopo katika ramani kuwa ni *miwili*. Katika kipengele cha mwisho (iv), baadhi ya wanafunzi waliweza kubaini alama inayowakilisha barabara, na kutaja idadi ya barabara zinazoelekea Kaskazini mwa kijiji. Wanafunzi hao walikuwa na ufahamu juu ya matumizi ya *dira* kwani walieleza kwa ufasaha idadi ya barabara zinazoelekea Kaskazini kuwa ni *moja*. Kielelezo Na. 4.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi swali la 4.


(i) Kuna shule ngapi katika kijiji cha Lumbila?

mbili.

(ii) Kanisa lipo upande gani toka kwenye daraja lililo karibu?

kusini.

(iii) Kuna milima mingapi katika kijiji cha Lumbila?

miwili.

(iv) Ni barabara ngapi zinaelekea Kaskazini mwa kijiji cha Lumbila?

moja.

Kielelezo Na. 4.2*: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi vipengele vinne vya swali la 4*

Wanafunzi wengi waliopata alama 6 walikosa kipengele cha (iv) kwani wengi wao waliandika *barabara mbili,* na wengine barabara *tatu*. Kwa ujumla, majibu hayo yasiyo sahihi yanaonesha kuwa wanafunzi hao walishindwa kutumia dira, hivyo hawakuweza kubaini idadi ya barabara zinazoelekea upande wa Kaskazini mwa kijiji. Kielelezo Na. 4.3 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshidwa kujibu kwa usahihi kipengele (ii) cha swali la 4.


(i) Kuna shule ngapi katika kijiji cha Lumbila?

Kuna shule mbili (2).

(ii) Kanisa lipo upande gani toka kwenye daraja lililo karibu?

Kutoka magharibi.

(iii) Kuna milima mingapi katika kijiji cha Lumbila?

Kuna milima miwili.

(iv) Ni barabara ngapi zinaelekea Kaskazini mwa kijiji cha Lumbila?

barabara moja (1).

Kielelezo Na. 4.3: *Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi kipengele cha (ii) cha swali la 4*

Kwa upande mwingine, wanafunzi 299,040 (19.1%) waliweza kujibu kwa usahihi vipengele 2 kati 4, hivyo kuwa na ufaulu wa wastani. Wanafunzi hawa walikuwa na uwezo wa wastani wa kusoma na kutafsiri ramani. Wengi wao walishindwa kujibu kwa usahihi kipengele (ii) na (iv). Katika kipengele (ii), wanafunzi wengi waliandika kanisa lipo upande wa Magharibi. Hii inaonesha kuwa wanafunzi hawa aidha walikosa stadi za kutosha juu ya alama za ramani inayowakilisha daraja, ama hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya dira. Kielelezo Na. 4.4 kinaonesha sampuli ya majibu

ya mwanafunzi aliyeshidwa kujibu kwa usahihi vipengele (ii) na (iv) vya swali la 4.


(i) Kuna shule ngapi katika kijiji cha Lumbila?

mbili.

(ii) Kanisa lipo upande gani toka kwenye daraja lililo karibu?

magharibi.

(iii) Kuna milima mingapi katika kijiji cha Lumbila?

Miwili.

(iv) Ni barabara ngapi zinaelekea Kaskazini mwa kijiji cha Lumbila?

one.

Kielelezo Na. 4.4: *Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi vipengele (ii) na (iv) vya swali la 4*

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, baadhi ya wanafunzi hawakuweza kujibu kwa usahihi kipengele hata kimoja, au walijibu kwa usahihi kipengele kimoja tu. Hivyo, wanafunzi 940,572 (60.3%) walipata alama 0 hadi 2. Hali hii inaonesha uwezo mdogo kabisa waliokuwa nao wanafunzi katika kutafsiri alama za ramani. Kati yao, wanafunzi 338,184 (21.7%) waliweza kujibu kipengele kimoja kwa usahihi kati ya vipengele vinne, na 602,388 (38.6%) waliandika majibu yasiyosahihi katika vipengele vyote. Wanafunzi hao walikosa maarifa ya kusoma na kutafsiri ramani. Kielelezo Na. 4.5 kinaonesha sampuli ya majibu ambayo si sahihi yaliyotolewa na mwanafunzi mmojawapo.



(i) Kuna shule ngapi katika kijiji cha Lumbila?

kuna shule tatu.

(ii) Kanisa lipo upande gani toka kwenye daraja lililo karibu?

kanisalipoupande wa shule.

(iii) Kuna milima mingapi katika kijiji cha Lumbila?

kunamilima mitatu.

(iv) Ni barabara ngapi zinaelekea Kaskazini mwa kijiji cha Lumbila?

Nibarabara mitano.

Kielelezo Na. 4.5: *Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu vipengele vyote katika swali la 4*

3.0 TATHIMINI YA KUFAULU KWA KILA UMAHIRI

Uchambuzi katika Upimaji wa Darasa la Nne (SFNA) 2021 unaonesha kuwa, kati ya mahiri kuu nne zilizopimwa (kama zilivyoainishwa kwenye muhtasari wa Elimu ya Msingi wa somo la Maarifa ya Jamii wa mwaka 2016), kiwango cha ufaulu kilikuwa kizuri katika mahiri mbili. Kiwango cha ufaulu kilikuwa cha wastani katika umahiri mmoja, na hafifu katika umahiri mwingine. Umahiri uliofanya vizuri zaidi ni *Kutambua Matukio Yanayotokea katika Mazingira Yanayomzunguka* ambao ulikuwa na ufaulu wa asilimia 82.8. Umahiri wa *Kufuata Kanuni za Kiuchumi katika Shughuli za Uzalishaji Mali* ulikuwa na ufaulu mzuri wa asilimia 70.7. Kwa upande mwingine, kiwango cha ufaulu katika umahiri wa *Kutumia Ramani na Elimu ya Anga katika Maisha ya Kila Siku* ulikuwa ni wa wastani kwa asilimia 39.7. Umahiri wa *Kutambua Misingi ya Uzalendo katika Jamii* ulikuwa hafifu kwa asilimia 28.5. Ijapokuwa wanafunzi wengi wameweza kupata umahiri unaokubalika katika mahiri tatu, bado wanafunzi hao wana upungufu wa umahiri

unaotarajiwa. Jedwali Na. 1 linaonesha mchanganuo wa kiwango cha ufaulu katika kila umahiri.

4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika maswali ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne 2021 katika somo la Maarifa ya Jamii umeonesha kiwango cha ufaulu cha umahiri mbili kuwa katika kiwango kizuri. Pia, uchambuzi zaidi umeonesha kiwango cha wastani katika umahiri mmoja na hafifu kwa umahiri mwingine. Aidha, kuna changamoto zilizosababisha baadhi ya wanafunzi wasifanye vizuri katika mahiri zilizotahiniwa. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na kushindwa kuelewa hitaji la maswali, ujuzi hafifu katika umahiri mahususi, na kushindwa kuhawilisha maarifa na ujuzi kutoka katika jamii inayomzunguka. Vilevile, baadhi ya wanafunzi walionesha uwezo mdogo wa kujua kusoma na kuandika, jambo lililosababisha ufaulu hafifu. Hali hii imejidhihirisha katika ufaulu wa swali la 3 linalohitaji stadi za kutosha za kusoma kwa uelewa na kuandika. Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi waliweza kuonesha umahiri wa kutosha uliowawezesha kubaini majibu sahihi katika maswali yaliyoulizwa na hivyo kuwa na utendaji mzuri.

5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuboresha kiwango cha utendaji wa wanafunzi, Baraza la Mitihani la Tanzania linapendekeza mambo yafuatayo:

(a) Walimu wasisitizwe kupima umahiri wa wanafunzi katika stadi za kusoma na kuandika, ili kuweza kuwasaidia wanafunzi walio na ujuzi mdogo wa kusoma kifungu cha habari na kubaini maudhui.

(b) Walimu watumie mbinu shirikishi mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji zinazolenga kukuza ujuzi wa ufahamu wa wanafunzi.

(c) Walimu wasisitizwe kufanya ziara za kimasomo maeneo mbalimbali yanayoweza kuwajengea wanafunzi kupata umahiri husika.

(d) Wanafunzi wapewe mazoezi ya kutosha yanayolenga kukuza umahiri na kuwajengea uwezo katika kujibu maswali yenye umahiri.

03 Maarifa ya Jamii - Ulinganifu wa ufaulu kwa wanafunzi katika kila umahiri kwa mwaka 2020 na 2021

	Umahiri	UPIMAJI 2020				UPIMAJI 2021			
		Ufaulu wa kila swali		Wastani wa ufaulu (%)	Maoni	Ufaulu wa kila swali		Wastani wa ufaulu (%)	Maoni
		Namba ya swali	% ya ufaulu			Namba ya swali	% ya a ufaulu		
1	Kutambua Matukio Yanayotokea Katika Mazingira Yanayomzunguka	2	67.34	67.34	Mzuri	1	82.80	82.80	Mzuri
2	Kufuata Kanuni za Kiuchumi Katika Shughuli za Uzalishaji Mali	1	68.40	66.41	Wastani	2	70.70	70.70	Mzuri
3	Kutambua Misingi ya Uzalendo Katika Jamii	3	66.41	66.41	Wastani	3	28.50	28.50	Hafifu
4	Kutumia Ramani na Elimu ya Anga Katika Maisha ya Kila Siku	4	66.37	66.37	Wastani	4	39.70	39.70	Wastani